

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA**

Simu: +255 026 23222761-5
Fax No. +255 026 2322624
E-mail: cna@bunge.go.tz



Ofisi ya Bunge,
10 Barabara ya Morogoro,
S.L.P. 941,
DODOMA.

TAARIFA KWA UMMA

Kamati tatu za Kudumu za Bunge zinawaalika wadau kutoa maoni kuhusu Itifaki mbili na Katiba ya Tume ya Afrika ya Usafiri wa Anga ya mwaka 2009 kabla Bunge halijapitisha Maazimio ya kuridhia Itifaki hizo na Katiba hiyo. Kamati zinazoshughulikia Itifaki hizo na Katiba hiyo ni pamoja na;

- **Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo;**

Itifaki ya Biashara ya Huduma ya Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika ya mwaka 2012 (SADC Protocol on Trade in Services, 2012).

Mkutano wa kupokea na kusikiliza maoni ya Wadau utafanyika siku ya Jumanne tarehe 22 Agosti, 2023 saa nne asubuhi katika Ukumbi wa Msekwa 'D', Ofisi ya Bunge Jijini Dodoma.

- **Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama;**

Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika wa Uingiaji na Utokaji wa Watu ya mwaka 2005 (The SADC Protocol on Facilitation of Movements of Persons, 2005).

Mkutano wa kupokea maoni ya wadau utafanyika siku ya Jumatano tarehe 23 Agosti, 2023 saa 8:00 mchana katika ukumbi wa Herman Sarwat, ghorofa ya tano jengo la Utawala, Ofisi ya Bunge Jijini Dodoma

- **Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu;**

Katiba ya Tume ya Afrika ya Usafiri wa Anga ya mwaka 2009 (The Constitution of the African Civil Aviation Commission, 2009).

Mkutano wa kupokea maoni ya wadau utafanyika siku ya Jumanne tarehe 22 Agosti, 2023 saa 8:00 mchana katika Ukumbi 231, ghorofa ya pili jengo la Utawala, Ofisi ya Bunge Dodoma.

Kamati zinawaalika wadau wote wenye maoni kuhusu Itifaki hizo na Katiba hiyo kufika na kuwasilisha maoni yao au kutuma kwa njia ya posta au barua pepe kwa anuani ifuatayo:-

Katibu wa Bunge,
Ofisi ya Bunge,
10 Barabara ya Morogoro,
S.L.P. 941,
40490 Tambukareli,
DODOMA.

Baruapepe:- cna@bunge.go.tz na kamati@bunge.go.tz . Itifaki hizo na Katiba hiyo zinaweza kupakuliwa katika tovuti ya Bunge ya <https://www.parliament.go.tz/resolutions-list>

Imetolewa na: Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa,
Ofisi ya Bunge,
10 Barabara ya Morogoro,
S.L.P 941,
DODOMA.

18 Agosti, 2023.